






# USCIS Inawakaribisha Wakimbizi na Waombaji Hifadhi ya Kisiasa

U.S. Citizenship and Immigration Services

M-1186-KIS (7/20)

# USCIS Inawakaribisha Wakimbizi na Waombaji Hifadhi ya Kisiasa

U.S. Citizenship and Immigration Services

# USCIS Inawakaribisha Wakimbizi na Waombaji Hifadhi ya Kisiasa

Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani (USCIS), ni sehemu ya Idara ya Usalama wa Ndani (DHS) ya Marekani, inakukaribisha Marekani kama mkimbizi au mwombaji hifadhi ya kisiasa. Tunathamini ujuzi na talanta zako, na tunataka kukusaidia kufanya makazi katika jamii yako na ufanikiwe kimaisha nchini Marekani. Pia tunataka kukupa maelezo kuhusu jinsi unavyoweza kuwa raia wa Marekani.

Brosha hii itakusaidia kujifunza kuhusu jinsi unavyoweza kuishi nchini Marekani na kuhusu haki, majukumu, na umuhimu wa uraia wa Marekani. Kuwa raia wa Marekani kunakupa haki sawia na Wamarekani wote na inaendeleza hali ya kushirikiana kwa pamoja kati yako na raia wenzako.



# Haki na Majukumu

Kama mkimbizi au mwombaji hifadhi ya kisiasa anayeishi nchini Marekani, una haki nyingi, kama tu watu wengine wanaoishi hapa. Baadhi ya haki hizi ni pamoja na uhuru wa kujieleza, uhuru wa dini, na uhuru wa mkusanyiko.

Pia una majukumu. Nchini Marekani, ni lazima kila mtu afuate sheria. Unahitaji kuelewa sheria za Marekani kwa sababu zinaweza kuwa tofauti na sheria za maeneo mengine ambapo umewahi kuishi. Kujifunza kuhusu historia, serikali, na utamaduni wa Marekani kutakusaidia kujihisi upo nyumbani hapa.

**Una haki ya:**

- Kuishi mahali popote nchini Marekani
- Kufanya kazi nchini Marekani
- Kuondoka na kurudi Marekani chini ya masharti fulani
- Kuhudhuria shule za umma hadi umri fulani, kulingana na sheria za jimbo
- Kutuma ombi la kadi ya Bima ya Kijamii isiyo na vikwazo
- Kutuma ombi la leseni ya udereva au aina nyingine ya kitambulisho cha serikali katika jimbo au himaya yako
- Kutuma ombi la kuwa mkazi halali wa kudumu na raia wa Marekani baada ya kustahiki
- Kuomba mke/mume wako au mtoto ambaye hajaoa/hajaolewa apate hadhi ya mwombaji hifadhi ya kisiasa au mkimbizi ili aishi nchini Marekani

- Kuripoti uhalifu au unyanyasaji kwa polisi na upate usaidizi wao

**Una jukumu na unatakiwa:**

- Kuomba ruhusa ya kurudi Marekani kabla ya kuondoka kwa kutuma ombi la hati ya kusafiria ya mkimbizi, hata kama wewe ni mwombaji hifadhi wa kisiasa
- Kutii sheria zote za serikali ya kitaifa, jimbo, na mitaa
- Kulipa kodi za serikali ya kitaifa, jimbo na mitaa, kama inatumika
- Kujisajili kwenye Selective Service (Huduma ya Uteuzi, huu ni wakala huru wa serikali ya Marekani ambao unahifadhi maelezo kuhusu uwezekano wa kujiunga na jeshi la Marekani) ikiwa wewe ni mwanaume mwenye umri wa kati ya miaka 18 na 26
- Kuwajulisha USCIS kuhusu anuani yako mpya na isizidi siku 10 baada ya kuhama makazi
- Kuwapeleka watoto wako shuleni
- Kutuma ombi la hadhi ya mkazi halali wa kudumu baada ya kuishi mwaka 1 nchini Marekani ikiwa wewe ni mkimbizi

## Kufanya Makazi nchini Marekani

Nchini Marekani, kila ngazi ya serikali ina jukumu tofauti katika mchakato wa kukusaidia kuishi vizuri. Unaweza kugusana na ofisi za serikali ya mitaa, jimbo, na kitaifa wakati wa mchakato wa kufanya makazi mapya.

Wasiliana na mratibu wako wa wakimbizi, mratibu wa afya ya wakimbizi, shirika la kusaidia wakimbizi kufanya makazi mapya au shirika la

kijamii ambalo linaloshirikiana na wakimbizi ili kukusaidia wewe kukuelekeza kwenye mpango maalumu wa usaidizi wa serikali. Mipango mingi ya usaidizi wa serikali ina muda mchache wa ustahiki ambao huanzia tarehe ambapo ulikubaliwa kama muomba hifadhi ya kisiasa au ulikubaliwa kama mkimbizi.



Ikiwa unahitaji msaada wa kujifunza Kiingereza, unaweza kujiandikisha kwenye darasa la Kiingereza. Wasiliana na wakala wako wa kufanya makazi mapya, maktaba ya umma, shirika la huduma za kijamii, au pahali pa kuabudu ili upate maelezo kuhusu madarasa ya Kiingereza na madarasa na huduma nyingine zilizopo.

## Hatua Zinazofuata Katika Mchakato Wako wa Uhamiaji

Ikiwa uliingia nchini Marekani kama mkimbizi ndani ya miaka 2 iliyopita au ulipewa hadhi ya mwombaji hifadhi ya kisiasa ndani ya miaka 2 iliyopita, unaweza kutuma ombi la jamaa fulani wa familia kujiunga nawe hapa. Unaweza kutuma ombi la jamaa wafuatao wa familia:

- Mume/Mke
- Mtoto (ambaye hajaoa/hajaolewa na ana umri wa chini ya miaka 21 mara

ya kwanza ulipotuma ombi la hadhi ya mwombaji hifadhi ya kisiasa au mkimbizi)

Ni lazima uwasilishe Fomu ya I-730, Ombi la Jamaa wa Mkimbizi/Mwomba Hifadhi ya Kisiasa kwa USCIS ndani ya miaka 2 ya kupewa ruhusa ya kuishi kama aliyepewa hifadhi ya kisiasa au kama mkimbizi, au uonyeshe sababu za kibinadamu za kuongeza kipindi cha miaka 2. Fomu hii inapatikana kwenye uscis.gov/i-730.

## Mkazi Halali wa Kudumu

Mkazi halali wa kudumu (Mmiliki wa Green Card) ni mtu aliyepewa idhini ya kuishi na kufanya kazi nchini Marekani kwa kudumu. Kama thibitisho la hadhi hiyo, mtu hupewa Kadi ya Mkazi Halali wa Kudumu, kwa kawaida inaitwa Green Card. Kupata Green Card kunakuweka kwenye njia ya kuwa na uwezo wa kuomba uraia kamili wa Marekani (maelezo zaidi kuhusu hili yanapatikana hapa chini).

- Ni **lazima** mkimbizi aombe Kadi ya Mkazi wa Kudumu mwaka 1 baada ya kufika nchini Marekani. Ni lazima mkimbizi awe amekuwepo nchini Marekani kwa mwaka 1 wakati wa kutuma ombi hilo.
- Mwenye kuomba hifadhi ya kisiasa **anaweza** kuomba Kadi ya Mkazi wa Kudumu mwaka 1 baada ya kupewa hifadhi ya kisiasa. Mwenye kupewa hifadhi ya kisiasa ni lazima awe amekuwepo nchini Marekani kwa mwaka 1 kama mwenye kupewa hifadhi ya kisiasa nchini Marekani wakati wa kutuma ombi hilo.

Ili kutuma ombi la hadhi ya Mkazi Halali wa Kudumu na kupata Kadi ya Mkazi wa

Kudumu, jaza Fomu ya I-485, Ombi la Kusajili Makazi ya Kudumu au Kubadilisha Hadhi. Fomu hii inapatikana kwenye uscis.gov/i-485. Ingawa kuna ada inayotozwa mwombaji hifadhi ya kisiasa kutuma ombi kwa kutumia Fomu ya I-485, hakuna ada inayotozwa mkimbizi kutuma ombi kwa kutumia Fomu ya I-485. Mashirika ya kijamii, ikiwemo wakala wa kufanya makazi mapya, wanaweza kukusaidia katika mchakato huu.

## Wakimbizi

Kama wewe ni mkimbizi, kwa mujibu wa sheria unatakiwa kutuma ombi la hadhi ya mkazi wa kudumu mwaka 1 baada ya kukubaliwa kuwa nchini Marekani kama mkimbizi.

**Kuomba makazi halali ya kudumu**

Tuma ombi kwa kutumia Fomu ya I-485, Ombi la Kusajili Makazi ya Kudumu au Kubadilisha Hadhi. Wakimbizi hawalipi ada ya kuwasilisha Fomu ya I-485 au ya kupokea huduma za bayometriki.

Unastahiki kutuma ombi ikiwa:

- Umekuwepo nchini Marekani kwa angalau mwaka 1 baada ya kukubaliwa kama mkimbizi;
- Umekuwepo nchini Marekani wakati wa kuwasilisha Fomu ya I-485;
- Umekubaliwa kuwa nchini Marekani kama mhamiaji; na
- Hadhi yako kama mkimbizi haijabatilishwa.

Tembelea uscis.gov/i-485 na uscis.gov/greencard/refugees ili kupata maelezo zaidi.

**Kuomba uraia wa Marekani**

Unaweza kustahiki kupata uraia kwa njia ya kuasili ikiwa umekuwa mkazi halali wa kudumu kwa idadi fulani ya miaka na kukidhi mahitaji mengine yote ya ustahiki.Tafadhali tembelea uscis.gov/citizenship ili kupata maelezo zaidi.

## Waombaji Hifadhi ya Kisiasa

Kama wewe ni mwombaji hifadhi ya kisiasa, unastahiki kuomba hadhi ya mkazi wa kudumu mwaka 1 baada ya kupewa hifadhi ya kisiasa ikiwa umedumisha makao yako kwa muda huo wote, lakini hauhitajiki kutuma ombi.

### Kuomba makazi halali ya kudumu

Tuma ombi kwa kutumia Fomu ya l-485, Ombi la Kusajili Makazi ya Kudumu au Kubadilisha Hadhi, na ulipe ada sahihi za uwasilishaji na huduma za bayometriki.

Unastahiki kutuma ombi:

- Umekuwepo nchini Marekani kwa angalau mwaka 1 baada ya kukubaliwa kupewa hifadhi ya kisiasa;
- Umekuwepo nchini Marekani wakati wa kuwasilisha Fomu ya I-485;
- Unaendelea kuwa na hadhi ya kuwa mkimbizi au mke/mume au mtoto wa mkimbizi;
- Hauna makazi ya kudumu katika nchi yoyote ya kigeni;
- Umekubaliwa kuwa nchini Marekani kama mhamiaji; na
- Hadhi yako kama mwombaji hifadhi ya kisiasa haijabatilishwa.

Tembelea uscis.gov/i-485 iyo uscis.gov/greencard/asylees ili kupata maelezo zaidi.

### Kuomba uraia wa Marekani

Unaweza kustahiki kupata uraia kwa njia ya kuasili ikiwa umekuwa mkazi halali wa kudumu kwa idadi fulani ya miaka na unatimiza mahitaji mengine yote ya ustahiki. Tafadhali tembelea Fadlan booqo uscis.gov/citizenship ili kupata maelezo zaidi.

# Uraia

Uraia ndicho kitu kinachowaunganisha pamoja Wamarekani wote. Marekani ni nchi ambayo haidumishwi kwa misingi ya mbari wala dini bali ni kwa misingi ya maadili yanayokubalika na Wamarekani wote kama vile uhuru na usawa. Kwa kuwa raia wa Marekani, utakuwa na msemo kuhusu jinsi taifa letu linavyoongozwa.

Tabia yako kama mkazi halali wa kudumu inaweza kuathiri uwezo wako wa kuwa raia wa Marekani hapo baadae. Mchakato wa kuwa raia wa Marekani unaitwa kuasili. Ni lazima utimize mahitaji yote ya ustahiki ili kuwa raia wa Marekani kwa njia ya kuasili.

Kwa ujumla, baada ya kukaa idadi fulani ya miaka kama mkazi halali wa kudumu, unaweza kutuma ombi la kuwa raia. Wakimbizi na waombaji hifadhi ya kisiasa wanaweza kuomba uraia miaka 5 baada ya kuwa wakazi halali wa kudumu. Waombaji hifadhi ya kisiasa hupewa idhini ya kuwa wakazi halali wa kudumu kuanzia tarehe ambayo ni mwaka 1 kabla ombi lao la Fomu ya I-485 kuidhinishwa. Baada ya Fomu ya I-485 kupata idhini, wakimbizi wanapata hadhi ya makazi halali ya kudumu kuanzia tarehe walipowasili nchini Marekani.



Ili kupata orodha ya mahitaji yote ya ustahiki wa uraia kwa njia ya kuasili, tembelea uscis.gov/citizenship. Baadhi ya mahitaji ni pamoja na yafuatayo:

- Unahitaji kuwepo nchini Marekani kwa kipindi cha muda fulani.
- Unahitaji kuwa na makazi endelevu nchini Marekani.
- Unahitaji kuwa na tabia njema.
- Unahitaji kuweza kuzungumza, kusoma, kuandika, na kuelewa Kiingereza cha kawaida na kufahamu historia na serikali ya Marekani (elimu ya utawala, kazi na haki za raia).
- Unahitaji kuunga mkono kanuni na maoni ya Katiba ya Marekani na uwe tayari kula kiapo cha uaminifu kwa nchi ya Marekani.



Ili kutuma ombi la uraia kwa njia ya kuasili, wasilisha Fomu ya N-400, Ombi la Usajili kwa Njia ya Kuasili, mtandaoni kwenye uscis.gov/n-400. Unaweza pia kulipa mtandaoni ada ya Fomu ya N-400 na huduma ya bayometriki. Kuna mambo yasiyofuata mkondo wa kawaida na mabadiliko katika mahitaji ya kuasili kwa wale wanaostahiki. USCIS pia hutoa msaada kwa watu wenye ulemavu.

Mashirika mengi ya kijamii, kama vile wakala wa kufanya makazi mapya, wanaweza kukusaidia kujitayarishia mchakato wa uraia kwa njia ya kuasili.

Manufaa fulani, haki, na majukumu yanaandamana na uraia wa Marekani, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kupiga kura katika uchaguzi wa serikali ya kitaifa, kuhudumu katika baraza la waamuzi katika mahakama, kusafiri ukitumia pasi ya Marekani, kushindania ajira katika serikali ya kitaifa, na kuwa afisa wa kupigiwa kura.

## Wasiliana na USCIS

Tembelea uscis.gov uscis.gov ili kupata maelezo zaidi, kukagua hadhi ya kesi yako, au kutafuta ofisi za USCIS. Unaweza kupiga simu kwa USCIS bila malipo kwa nambari 800-375-5283. Kwa watu ambao ni viziwi, wenye upungufu wa kusikia au wana ulemavu wa usemi, piga simu TTY kwa nambari 800-767-1833. Huduma inapatikana kwa Kiingereza na Kihispania. Pia unaweza kutembelea uscis.gov/contactcenter ili kuwasiliana na Kituo cha Mawasiliano cha USCIS.

### Rasilimali za USCIS

**Huduma za Uraia na Uhamiaji za Marekani (USCIS)**

USCIS inasimamia uhamiaji halali nchini Marekani. Jifunze jinsi ya kutuma ombi lako la kupata Green Card, fuatilia uraia wa Marekani, ungana na familia, pata idhini ya kusafiri nje ya nchi, na mengine mengi.

Rasilimali kwa wakimbizi na waombaji hifadhi ya kisiasa
uscis.gov/howdoi/refugeesasylees

## Rasilimali za USCIS

**Karibu Marekani: Mwongozo kwa Wahamiaji Wapya**

Mwongozo huu unatoa maelezo msingi ambayo wewe na familia yako mnahitaji katika maisha ya kila siku nchini Marekani. Unaelezea haki na majukumu yako, unapendekeza maoni ya jinsi ya kushiriki katika jamii yako, na kukusaidia kufanya mipango ya kuomba uraia wa Marekani wakati utakapokuwa mkazi halali wa kudumu.

uscis.gov/newimmigrants

**Kufanya Makazi Nchini Marekani**

Ukurasa huu wa tovuti unakupa maelezo kuhusu Marekani, elimu na utunzaji watoto, dharura na usalama, kusafiri nje ya Marekani, ajira, kufanya makazi nchini Marekani, manufaa ya serikali, huduma za afya, na pesa na uchumi.

uscis.gov/tools/settling-us

**Kituo cha Rasilimali za Uraia**

Tovuti hii inatoa zana za kielimu na taarifa za kukusaidia kujiandaa kupata uraia wa Marekani.

uscis.gov/citizenship

**Epuka Utapeli**

Ikiwa unahitaji msaada wa kisheria kuhusiana na masuala ya uhamiaji, hakikisha mtu ambaye anakusaidia ameidhinishwa kutoa ushauri wa kisheria. Ni wakili au mwakilishi tu aliyeidhinishwa anayefanya kazi katika taasisi inayotambuliwa na Idara ya Sheria ya Marekani anaweza kukupa ushauri wa kisheria.

uscis.gov/avoid-scams
uscis.gov/avoid-scams/find-legal-services

## Rasilimali za USCIS

### Fomu

Tumia **Fomu ya I-765** kutuma ombi la idhini ya kazi, kuweka upya idhini yako, au kubadilisha hati yako.

uscis.gov/i-765

Tumia **Fomu ya I-730** kumleta mke/mume wako au watoto wako nchini Marekani.

uscis.gov/i-730

Tumia **Fomu ya I-131** kutuma ombi la ruhusa ya kurudi nchini Marekani kwa kupata hati ya kusafiria ya wakimbizi.

uscis.gov/i-131

Tumia **Fomu ya I-485** kutuma ombi la hadhi ya kuwa mkazi halali wa kudumu kama upo nchini Marekani.

uscis.gov/i-485

Tumia **Fomu ya N-400** kutuma ombi la uraia wa Marekani.

uscis.gov/n-400

Tumia **Fomu ya AR-11** kuhakikisha anuani yako imesasishwa na USCIS.

uscis.gov/ar-11

### myUSCIS

Pata maelezo ya hivi sasa zaidi kuhusu mchakato wa ombi la kupata manufaa ya uhamiaji, zana za kukusaidia kujiandaa kwa ajili ya mchakato wa uraia kwa kuasili, na rasilimali za kutafuta madarasa ya maandalizi ya uraia na madaktari katika jamii yako. Jifunze jinsi ya kutuma ombi mtandaoni na ufikiaji maelezo kuhusu kesi yako kwa kusajili akaunti mtandaoni.

my.uscis.gov
myaccount.uscis.dhs.gov

# Rasilimali Nyingine za Serikali ya Kitaifa

Chati ifuatayo inatoa maelezo ya ziada kuhusu huduma za serikali ya kitaifa kwa wakimbizi na waombaji hifadhi ya kisiasa.

| Rasilimali za Serikali ya Kitaifa |
| --- |
| **Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani**<br>**Utawala wa Watoto na Familia**<br>**Ofisi ya Kuwapa Wakimbizi Makazi Mapya (ORR)**<br>Ikiwa wewe ni mkimbizi, mwombaji hifadhi ya kisiasa, na jamaa wa familia ya mtu husika, unaweza kustahiki kupokea msaada na huduma kupitia ORR. ORR inadhamini na kusimamia mipango tofauti tofauti ikiwemo misaada ya fedha na kimatibabu, maandalizi ya ajira, kupewa ajira, na mafunzo ya lugha ya Kiingereza. Mipango hii ina ustahiki wa muda fulani ambao huanza tarehe uliyoidhiniswha kupata hifadhi ya kisiasa au tarehe ulipoingia nchini Marekani kama mkimbizi. ***Unapaswa kuchunguza kama unastahiki kwa mpango wowote kati ya mipango hiyo punde iwezekanavyo ikiwa una nia yoyote katika mpango wowote.***<br>**Waratibu wa wakimbizi wa jimbo/Waratibu wa jimbo wa afya ya wakimbizi**<br>acf.hhs.gov/orr/resource/orr-funded-programs-key-contacts<br>**Mipango na rasilimali za jimbo**<br>acf.hhs.gov/orr/state-programs-annual-overview<br>**Rasilimali za bima ya afya**<br>acf.hhs.gov/orr/health<br>**Rasilimali za makazi ya bei nafuu**<br>acf.hhs.gov/orr/resource/finding-affordable-housing<br>**Rasilimali za ajira**<br>acf.hhs.gov/orr/employment-resources |

## Rasilimali za Serikali ya Kitaifa

**Idara ya Taifa ya Marekani**
**Ofisi ya Idadi ya Watu, Wakimbizi, na Uhamaji**
**Mpango wa Mapokezi na Kupangwa**

Ikiwa umepewa hadhi ya mkimbizi nchini Marekani, ulifadhiliwa na wakala wa kufanya makazi mapya ambao unashiriki katika Mpango wa Mapokezi na Kupangwa, ambao ni mpango unaosimamiwa na Idara ya Taifa ya Marekani. Wakala unaodhamini una wajibu wa kukuandikisha katika mojawapo ya ofisi zao na kukupa huduma za mwanzo, kama vile makazi, vyombo muhimu vya nyumbani, chakula, mavazi, maelekezo na msaada wa ufikiaji wa huduma nyingine za kijamii, matibabu, na ajira wakati wa siku zako 30 hadi 90 za kwanza nchini Marekani. ***Mara ya kwanza unapowasili nchini Marekani kama mkimbizi, wakala wako wa kufanya makazi mapya ndio utakuwa mahali pako pa kwanza kukimbilia unapohitaji msaada wa kufanya makazi.***

state.gov/refugee-admissions/reception-and-placement

**Idara ya Taifa ya Marekani**
**Ofisi ya Idadi ya Watu, Wakimbizi, na Uhamaji**
**Ubadilishaji Rasilimali za Mwelekeo wa Kitamaduni (CORE)**

Unafadhiliwa na Idara ya Taifa ya Marekani, CORE inatoa rasilimali nyingi za kitamaduni kwa wakimbizi wanaotarajiwa kuwasili nchini Marekani. Tovuti hii inajumuisha nyenzo kwa lugha kama vile Kiarabu, Kifarsi, Kinyarwanda, Kiswahili, na Kisomali. CORE itakupa maelekezo ya kitamaduni nchini Marekani. ***Tembelea CORE sasa ili ujifunze mengi zaidi kuhusu ajira, makazi, afya, udhibiti pesa, na mengine mengi ili kukusaidia kuzoea maisha nchini Marekani.***

corenav.org

## Rasilimali za Serikali ya Kitaifa

**Idara ya Leba (DOL) ya Marekani**

DOL inabuni, inakuza, na kuendeleza maslahi ya wafanyakazi, wanaotafuta kazi, na waliostaafu wa Marekani; inafanya kazi ili kuimarisha fursa za kupata ajira inayolipa vizuri; na kudumisha manufaa na haki zinazohusiana na kazi. ***Tazama careeronestop.org. Inaweza kukusaidia kupata kazi na mafunzo katika jamii yako.***

**Rasilimali za haki za Wafanyakazi**

dol.gov

**Vituo vya Ajira vya Marekani (kimedhaminiwa na DOL)**

careeronestop.org

877-US2-JOBS (877-889-5627 (TTY))

**Idara ya Sheria ya Marekani Kitengo cha Haki za Wahamiaji na Wafanyakazi**

Kitengo cha haki za Wahamiaji na Wafanyakazi katika Idara ya Sheria ya Marekani kinadumisha kifungu cha kupinga ubaguzi cha Sheria ya Uhamiaji na Utaifa (Immigration and Nationality Act). Sheria hii inazuia waajiri kubagua kwa misingi ya hadhi ya uraia na asili ya utaifa wakati wa kuajiri, kusitisha ajira, au kutafuta waajiriwa au kutoza ada ya mapendekezo. ***Pia inazuia vitendo visivyo vya haki vya kulipiza kisasi au kutoa vitisho. Ikiwa unafikiri hautendewi haki unapojaribu kutafuta ajira au katika ajira ambapo unafanya kazi kwa sababu ya unakotoka, au kwa sababu wewe ni mwombaji hifadhi ya kisiasa au mkimbizi, Sehemu ya Haki za Wahamiaji na Wafanyakazi inaweza kusaidia.***

**Rasilimali kuhusu ubaguzi wa ajira kwa misingi ya uraia au hadhi ya uhamiaji**

justice.gov/crt/immigrant-and-employee-rights-section

800-255-7688 (800-237-2515 (TTY))

## Rasilimali za Serikali ya Kitaifa

### Idara ya Hifadhi ya Jamii

Namba ya **Bima ya Kijamii** inahitajika ili kupata ajira, kuchukua manufaa ya Bima ya Kijamii, na kutuma maombi ya huduma nyiingine za serikali. ***Unahitajika kupata namba na kadi ya Bima ya Kijamii. Nenda kwenye tovuti hii ili kupata maelezo mahsusi ya wakimbizi na waombaji hifadhi ya kisiasa.***

ssa.gov/people/immigrants

800-772-1213 (800-325-0778 (TTY))

USCIS imenunua haki za kutumia picha nyingi zilizo kwenye *USCIS Inawakaribisha Wakimbizi na Waombaji Hifadhi ya Kisiasa.* USCIS imepewa leseni ya kutumia picha hizi kwa machapisho yasiyo ya kipekee na kwa njia isiyohamishika. Haki nyingine zote za picha hizi, zikiwemo bila mipaka na hakimiliki, zinasalia na mmiliki wa picha hizo. Picha hizi hazipayikani hadharani na haziwezi kutumika ila kama vinavyotokea kama sehemu ya chapisho hili.

U.S. Citizenship and Immigration Services

uscis.gov